**HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**

**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 20.04.2017 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**

**WALIOHUDHURIA**

**WAH. MADIWANI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh.Ahmadi S. Makoroganya | - Ugawaji – Mwenyekiti H/W | - Mwenyekiti |
| 2. Arbogast T. Kiwale | - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | - Katibu |
| 3. Mh.Issaya M. Ndwewe | - Mitumbati- M/Mwenyekiti H/W | - Mjumbe |
| 4. Mh.Monica Kasembe | - Viti Maalum Nambambo | - Mjumbe |
| 5. Mh.Abdallah M. Nkane | - Nditi | - Mjumbe |
| 6. Mh.Adinani A. Mpyagila | - Mbondo | - Mjumbe |
| 7. Mh.Abdallah A. Saidi | - Nachingwea | - Mjumbe |
| 8. Mh.Omari A. Chitanda | - Nangowe | - Mjumbe |
| 9. Mh.Anton S. Lalo | - Namatula | - Mjumbe |
| 10. Mh.Asha J. Mdamo | - Nachingwea Viti Maalum | - Mjumbe |
| 11. Mh.Asina A. Rutumbo | - Ngunichile Viti Maalum | - Mjumbe |
| 12. Mh.Beatrice B. Lilungulu | - Mnero Ngongo Viti Maalum | - Mjumbe |
| 13. Mh.Catherine B. Kapanda | - Nachingwea Viti Maalum | - Mjumbe |
| 14. Mh.Elice J. Chitumbi | - Chiola Viti Maalum | - Mjumbe |
| 15. Mh.Emanuel A. Mhagama | - Namikango | - Mjumbe |
| 16. Mh.Ereneus H. Kambona | - Boma | - Mjumbe |
| 17. Mh.Filbert F. Mnali | - Mtua | - Mjumbe |
| 18. Mh.Jamali F. Tamba | - Mpiruka | - Mjumbe |
| 19. Mh.Gabriel D. Matuta | - Naipanga | - Mjumbe |
| 20. Mh.Gervas B. Ungele | - Mnero Miembeni | - Mjumbe |
| 21. Mh.Hamida A. Hassani | - Ngunichile Viti Maalum | - Mjumbe |
| 22. Mh.Hamisi H. Chinguile | - Kilimarondo | - Mjumbe |
| 23. Mh.Hamisi M. Kalembo | - Mkoka | - Mjumbe |
| 24. Mh.Hamisi M. Nyassa | - Ndomoni | - Mjumbe |
| 25. Mh.Hemed S. Madogo | - Kiegei | - Mjumbe |
| 26. Mh.Ignas P. Kupangwa | - Ruponda | - Mjumbe |
| 27. Mh.Joachim D Nnungu | - Lionja | - Mjumbe |
| 28. Mh.Joyce B. Mtauka | - Ruponda Viti Maalum | - Mjumbe |
| 29. Mh.Khamisi R. Majamba | - Chiola | - Mjumbe |
| 30. Mh.Lusia C. Mchopa | - Naipingo Viti Maalum | - Mjumbe |
| 31. Mh.Mchinge M. Mchopa | - Kilimanihewa | - Mjumbe |
| 32. Mh.Matilde L. Milopa | - Kipara Mtua | - Mjumbe |
| 33. Mh.Mohamed S. Mbemba | - Nambambo | - Mjumbe |
| 34. Mh.Omari A. Mbinga | - Mnero Ngongo | - Mjumbe |
| 35. Mh.Omari M. Lingumbende | - Namapwia | - Mjumbe |
| 36. Mh.Paulina S. Mchopa | - Stesheni | - Mjumbe |
| 37. Mh.Rabia J. Penengu | - Mchonda | - Mjumbe |
| 38. Mh.Saada Y. Makotha | - Mkotokuyana | - Mjumbe |
| 39. Mh.Abdallah A. Mkamate | - Kipara Mnero | - Mjumbe |
| 40. Mh.Saida K. Nahoma | - Nachingwea Viti Maalum | - Mjumbe |
| 41. Mh.Saidi B. Makayola | - Ngunichile | - Mjumbe |
| 42. Mh.Abilahi S. Manyamba | -Naipingo | -Mjumbe |
| 43. Mh.Simon P. Mkwalila | - Nang`ondo | - Mjumbe |
| 44. Mh.Selemani A. Mbinga | -Marambo | -Mjumbe |
| 45. Mh.Veronica D. Makotha | - Mpiruka Viti Maalum | - Mjumbe |

46. Mh.Emanuel K. Kinaki - Matekwe - Mjumbe
47. Mh.Hadija I. Komba - Matekwe Viti Maalum - Mjumbe

**WATALAAM**

1. Mohamedi Mnunguye - Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
2. Abilahi Raskombe - Kaimu Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Mji Mdogo
3. Msafiri Tematema - Kaimu Mkuu wa idara ya maji
4. John D. Masika - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto
5. Leonard Mkwela - Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
6. Kenneth A. Mwangama - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
7. Geofrey Nnauye - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
8. Athuman H. Mnyusi - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi
9. Oliver P. Nyaki - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
10. Jabiri M. Ndagula - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki
11. Lazaro Dotto - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
12. James Mbakile - Mratibu wa TASAF
13. Mohamed Mnali - Kaimu Afisa Biashara
14. Abdallah Membe - Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
15. Gregory Matandiko - Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
16. Theogen Rutale - Mratibu wa Mikopo Mfuko wa Wanawake na Vijana
17. Fatuma Milao - Mratibu wa UKIMWI
18. Tunu H. Goagoa - Kaimu Afisha Ushirika
19. Raphael Y. Ajetu - Mkuu wa Idara ya Kilimo Umwagiliaji na Ushirika
20. Mussa D. Mumina - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji
21. Daniel Bhoke - Kaimu Afisa Ardhi (W)
22. Samwel Laurence Msaki - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
23. Joseph E. Ntomela - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
24. Rashid S. Amuri - Afisa Tarafa Kilimarondo
25. Ernest Ng'onye - Kaimu Afisa Tarafa Lionja
26. Benjamin Ndumbaro - Kaimu Afisa Tarafa Naipanga
27. Ally Mkitage - Kaimu Afisa Tarafa Nambambo
28. Jeremia A. Muwefu - Afisa Tarafa Ruponda
29. Bihaga Yogwa - Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
30. Martha Kambona - Mwandishi wa Mikutano
31. Juma A. Mkopi - Mwandishi wa Mikutano

**WAALIKWA**

1. Rukia Muwango - Mkuu wa Wilaya
2. Albert Mnali - Mwenyekiti wa CCM (W)
3. Leticia Mtimba - Katibu wa CCM (W)
8. Mustaph Muni - Mwenyekiti Mamlaka ya Mji mdogo

**WASIOHUDHURIA**

1. Mh. Elias Hassan Masala -Mbunge Mjumbe kwa taarifa

**HWN/MBK/ MUHTASARI NA 97/2017 KUFUNGUA MKUTANO**

Katibu alianza kwa kusema kuwa huo ulikuwa ni mkutano wa Baraza la Madiwani. Mkutano wa kawaida kulingana na kalenda ya Halmashauri Katibu aliendelea kusema kuwa akidi ya wajumbe imetimia ndipo alipomkaribisha Mwenyeiti ili afungue Mkutano. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe Wataalam na waalikwa kwenye Mkutano huo wa Baraza la Madiwani robo ya tatu mwaka wa fedha 2016/2017. Mwenyekiti

aliwajulisha wajumbe kuwa katikakila Halmashauri hufanya mkutano wa Baraza kila miezi mitatu na hii ni robo ya tatu kwa ajili ya Baraza kujadili taarifa ambazo pia zimejadiliwa kwenye vikao vya kamati za kudumu na kuwa ni imani yake wajumbe watafuata taratibu kwa kuhoji taarifa ya kamati zingine. Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua Mkutano saa 5:30.

**HWN/MBK/MUHTASARI NA 98/2017 KUTHIBITISHA AGENDA**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe katika kuzipitia ajenda za Mkutano hatimaye wajumbe walizikubali kwa ajili ya kuzijadili.

**HWN/MBK/ MUHTASARI NA 99/2017 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 27.01.2017 NA 07.02.2017**

Mihtasari ilisomwa na kupokelewa Mwenyekiti na Katibu walitia saini zao kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi za Mikutano hiyo.

**HWN/MBK/ MUHTASARI NA 100/2017 YATOKANAYO**

**YATOKANAYO MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI LILOFANYIKA TAREHE 27.01.2017**

| MUH NA. | AZIMIO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 86/2017 | Takwimu kwa mazao ya Ufuta, Mbaazi na Korosho; CMT ifuatilie kupata takwimu sahihi za mazao ya Mbaazi na Ufuta. | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Taarifa ilitolewa kwenye mkutano |

**Takwimu ya Mazao;** Wajumbe walipitia taarifa/ takwimu za mazao kwa vyama vya Msingi msimu wa 2016/2017 kwa mazao ya Ufuta, Mbaazi na Korosho ambapo takwimu zilionyesha chama cha KINANA uzalishaji wake upo chini kwa mazao yote hii ni kusema Chama hicho hakitakuwa na uwezo wa kujiendesha, katika kujadili hoja hiyo wajumbe walisema na kukubaliana chama hicho kifutwe kwa sababu ya kuwa na uzalishaji mdogo.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kwa ushauri kuwa sheria zipo lakini inawezekana kushauri vyama viunganishwe ili kuvifanya vyama kuwa na nguvu ya kiuchumi kuliko uamuzi wa kukifuta chama.

Wajumbe walizungumzia hoja ya chama cha KINANA njia iliyotumika katika kupata usajili, ambapo walikubaliana kutokana na chama hicho kuwa na Takwimu ndogo ya makusanyo yake hivyo chama hicho kirudi Matekwe AMCOS ili chama kiwe na nguvu.

Wajumbe walijadili hoja ya chama cha KINANA kwa kusema chama hicho kifutwe kwa sababu eneo lake hakuna uzalishaji wa kutosha, kama Halmashauri iliweka taratibu chama cha Msingi kiwe na uwezo wa kukusanya mazao kufikia tani mia tatu (300) na kuwa takwimu zinaonyesha chama cha KINANA kipo chini hivyo chama hicho kifutwe.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kuwa hoja ya kufuta chama hatua zake ni kubwa, na Baraza halina mamlaka wa kufuta Chama ila inaweza kutoa ushauri kwa vyombo husika.

**Azimio;** Halmashauri imwandikie barua Mrajisi wa Ushirika Mkoa kushauri kukifuta chama cha Msingi cha KINANA baada ya kuonekana takwimu zake za uzalishaji zipo chini.

**Salamu za Mkuu wa Wilaya;**Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuwa kumetokea mwingiliano wa shughuli ambapo Mkuu wa Wilaya mbali na kuhudhuria Mkutano huo, bado anatarajia kuwapokea wageni kamati ya ulinzi na usalam Mkoa ikiongozwa na Mwenyekiti wao ambaye ni Mkuu wa Mkoa ambapo wanakuja kwa ajili ya kuzungukia miradi itakayopitiwa na Mwenge. Kutokana na hilo Mkuu wa Wilaya ataungana na ugeni huo

hivyo Mwenyekiti aliomba kwa wajumbe kumpa nafasi Mkuu wa Wilaya ili atoe nasaha zake. Mkuu wa Wilaya alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kumwezesha kuhudhuria Mkutano huo wa Baraza, aliendelea kutoa shukrani kwa Wah. Madiwani katika kutekeleza majukumu yao kwa dhati.

**Maagizo ya Serikali;** Mkuu wa Wilaya alisema mvua zimenyesha za kutosha na wakulima wamepata mazao na mavuno ya mahindi yameanza ambapo alisema wakulima wadhibitiwe wasiuze kiholela mahindi mabichi, kitendo hicho kinatishia kuwepo na upungufu wa chakula. Mkuu wa Wilaya alisema walikaa na wafanyabiashara ambao walisema bei ya vyakula imepanda Sokoni ambapo pia hali hiyo imechangiwa na uharibifu wa barabara.

**Mauzo ya Korosho;** Mkuu wa Wilaya alizungumzia mauzo ya korosho msimu wa 2016/2017, kwa kushukuru bei ilikuwa nzuri kwa wakulima, ambapo ilikidhi mahitaji mbalimbali ya wakulima. Mkuu wa Wilaya alisema kulikuwepo na changamoto kwa chama kikuu cha RUNALI na vyama vya wakulima ambavyo baadhi yake havijalipa wakulima fedha za mauzo ya korosho, Mkuu wa Wilaya alitaka wakulima hao walipwe fedha zao. Mkuu wa Wilaya pia alizungumzia mazao ya Ufuta na Mbaazi kwa kusema bado kuna changamoto ya kushuka kwa bei ya kuuza kwa mkulima na kusema kuwa tarehe 21.04.2017 kutafanyika kikao Mkoani kwa ajili ya kudhibiti mporomoko wa bei ya mazao hayo.

**Elimu na Afya;** Mkuu wa Wilaya alisema Serikali ya Wilaya imebaini kuwepo na matatizo kwenye sekta hizo, kuhusu Elimu Mkuu wa Wilaya alizungumzia suala la ufaulu kwa wanafunzi na kuwa jambo hilo linategemea ushirikiano wa wazazi , walezi na wanafunzi wenyewe ambapo Mkuu wa Wilaya aliwaomba Wah. Madiwani ambao ni wenyeviti wa kamati za maendeeo za Kata wasimamie suala la kudhibiti vitendo vya utoro wa rejareja ambavyo kwa mwanafuzi akiachiwa hufikia hatua ya kuacha shule.

Mkuu wa Wilaya alizungumzia shule ambazo hazikufuata taratibu katika kusajiliwa, shule ambazo zimefanya kazi miaka mitatu (3) na kuwa hilo limeonwa na kuwa hatujachelewa katika kulirekebisha ili kufuata taratibu zinazopasika.

**Upande wa Afya;** Mkuu wa Wilaya alisema kuna changamoto ambapo 30% ya watumishi wake ndio wameajiriwa, na Serikali inashughulikia katika kupunguza tatizo la watumishi wa Sekta hiyo. Mkuu wa Wilaya pia alisema, ndani ya Wilaya kuna mtu alikuwa anafanya shughuli za kitabibu bila kufuata taratibu, kwenye eneo hilo wapo wananchi walitibiwa na kupona, kufikia hali hiyo haikuachwa hivyo na kuwa Serikali imechukua hatua ambapo muhsika amekamatwa.

**Ulinzi na Uslama;** Mkuu wa Wilaya alizungumzia hali ya Ulinzi na Usalama kuwa imeimarika ambapo ndani ya Wilaya hakuna hali ya kutishia usalama. Wilaya imekuwa inafuatilia na kudhibiti masuala ya madawa ya kulevya ambapo msako umefanyika na kukamata viloba vya pombe

**Mwenge wa Uhuru;** Mkuu wa Wilaya aliwaomba Wah. Madiwani waende kutoa hamasa na kuwaomba wananchi wachangie Mwenge, aidha wananchi washiriki katika kuushangilia Mwenge wakati wa kuupokea, na kuukimbiza Mwenge utakapokuwa Wilayani. Mkuu wa Wilaya pia alisisitiza kutoa michango, mwenge unaangalia kiasi gani cha mchango kimechangiwa ili kufanikisha suala zima la mwenge. Mwisho Mkuu wa Wilaya alitoa shukrani kwa kumsikiliza.

**<u>HWN/MBK/MUHTASARI NA 101/2017 MAMBO YANAYOHUSU SHERIA</u>**

**1. Mapendekezo ya Sheria Ndogo za kodi ya Majengo za Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea za mwaka 2017**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria aliwasilisha mapendekezo ya Sheria Ndogo za kodi ya Majengo za Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea za mwaka 2017, taarifa ilieleza kuwa hadi kufikia tarehe 04/04/2017

jumla ya kata 22 kati ya 31 zilikuwa zimewasilisha mihtasari yenye mapendekezo ya mapitio ya Sheria ndogo ya kodi ya majengo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea.

Aidha, miongoni mwa kata hizo kata zilizoridhia mapendekezo ya Sheria hii ni 16 kati ya kata 22 zilizowasilisha mihtasari ya Sheria ndogo ni hizi. Sheria ndogo ili iweze kupitishwa inahitajika nusu ya kata zote za Halmashauri kuridhia na kwa kuwa jumla ya kata zilizopelekewa mihtasari hii zilikuwa 31 na kata zilizoridhia ni kata 16 hivyo kuwa nusu ya kata zote.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavyo;

**Wajibu wa kusajili;** mjumbe alianza kwa kusema kuwa rasimu ya Sheria zimepwaya, mjumbe haoni sababu ya mmiliki wa Jengo apate kazi kumfuata mtaalam kwa ajili ya kusajili jengo ambapo mjumbe alipendekeza kazi hiyo ifanywe na Halmashauri kuhakikisha majengo yote yatakayolipiwa kodi yanasajiliwa.

Eneo lingine ambalo wajumbe walilizungumzia ni eneo la vijijini ambako majengo yake yapo kwenye viwanja ambavyo havijapimwa, ambapo kwenye maeneo hayo kodi itatozwa, lakini limetajwa suala la malimbikizo ni kwa muda gani mmiliki atatakiwa kulipa kodi ya malimbikizo.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kuwa mlipa kodi anatakiwa kutoa ushirikiano katika kusaidia Halmashauri kukusanya mapato yake na kuwa haitaondoa wajibu wa mtaalam katika jambo hilo.

Muda wa malimbikizo ni baada ya kwisha mwaka uliotakiwa mlipa kodi alipie na kuwa baada ya muda huo mmiliki wa jengo atatakiwa kulipa na malimbikizo.

Mjumbe alichangia kwa kusema kuwa Halmashauri ina kazi kabla ya kupitisha sheria, inapaswa kutolewa elimu kwanza kwa wananchi ili wajue sheria hiyo itakavyokuwa inafanya kazi.

Wajumbe walijulishwa kuwa elimu itatolewa kwa wananchi wetu juu ya ulipaji wa kodi ya majengo ikizingatiwa kuwa mpango wa ulipaji kodi ya majengo tayari umeshaingia kwenye mpango wa bajeti ya Halmashauri 2017/2018, maelezo mengi yametolewa kuhusu kodi ya majengo na kuomba sheria hiyo ipite na elimu itaendelea kutolewa kwa sababu elimu ni kitu endelevu.

Katika kuchangia hoja hiyo mjumbe alisema sheria iangalie isije Halmashauri ikatumia gharama kubwa, na mapato katika Halmashauri yakawa madogo ambapo mjumbe aliomba sheria hiyo irudi kwa wananchi wapate elimu kabla ya kuanza kutumika.

Wajumbe walikubaliana sheria hiyo ipite na waangalie mapendekezo yaliyotolewa kwenye Kata na kuomba viwango vilivyokadiliwa vipungue.

**Azimio;** kwamba wajumbe walipitisha sheria ndogo za kodi ya majengo za Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea.

**2. Mapendekezo ya uanzishwa wa sheria ndogo ya Mfuko wa Maendeleo ya huduma za Jamii.**

Kaimu Mkuu wa kitengo cha Sheria aliwasilisha rasimu ya Sheria ndogo ya Mfuko wa maendeleo ya Huduma za Jamii ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kwa mwaka 2017. Kwa mujibu wa Sheria ndogo hiyo Halmashauri inategemea kupata mchango kwa kukata shilling 30 kwa kilo kwenye zao la biashara (korosho) kwa lengo la uboreshaji wa huduma za jamii (Elimu na Afya na Kilimo).
Shilling 30 inayotegemewa kukatwa kwenye kila kilo ya korosho ambayo itagawanywa kwa mchanganuo ufuatao; Shilling 15 itabaki Halmashauri kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za jamii (Afya na Elimu). Sh.8-elimu na sh.7 –afya, Shilling 5 hii itabaki Kijijini kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za maendeleo ya Kijiji, Shilling 5 hii itabaki kwenye kata kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli maendeleo za kata na Shilling 5 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu bora.

Taarifa ilipokelewa nakujadiliwa kama ifutavyo

Wajumbe walichangia kwa kukubali kuanzishwa kwa sheria ndogo ya Mfuko wa Maendeleo ya huduma za Jamii kuwa Tsh. 15/= ibaki Halmashauri kwa ajili ya uboreshaji huduma za Jamii, Afya na Elimu kama mapendekezo yalivyo na mgao uwe sawa fedha hizo zikafanye kazi sawa kwenye Kata zote na kusisitizwa mgao wake uende sawa kwa eneo la Kata , vijiji na ununuzi wa pembejeo.

Mgao ni kama ifuatavyo kata Tsh. 7/= kijiji Tsh. 6/= ununuzi wa Tsh. 2/= ambapo wajumbe walikubaliana wataenda kuelezea kwa wananchi ili sheria hiyo ieleweke na kukubaliwa na wananchi.

**Azimio;** uanzishwaji wa Sheria Ndogo ya Mfuko wa Maendeo ya huduma za Jamii Mgao wa fedha Tsh. 30/= kuwa ni Elimu Tsh. 8/= na Afya Tsh. 7/=maendeleo ya Kata Tsh. 7/= maendeleo ya kijiji Tsh. 6/= ununuzi wa Mbegu bora Tsh. 2/= Rasimu ipelekwe kwa wananchi kupata maoni yao.

## HWN/MBK/MUHTASARI NA. 102/2017 KUPOKEA TAARIFA ZA KAMATI NA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU

### 1. Kamati ya Fedha , Uongozi na Mipango

Mwenyekiti wa Kamati, alitoa ripoti na kuwasilisha mihtasari ya vikao vya tarehe 14.01.2017, 23.02.2017 na tarehe 30.03.2017 ambayo imethibitishwa.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavyo.

**Maombi ya kuuzwa gari STK 4729 Land Cruiser V8**

Mjumbe baada ya kupitia taarifa ya mihtasari ya kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango alisema haungi mkono hoja ya kuuzwa kwa gari la Mkurugenzi Land Cruiser V8 na kupendekeza sasa gari hilo litengenezwe na Halmashauri ili lifanye kazi. Aidha gari hilo akabidhiwe Mwenyekiti wa Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

**Taarifa za Kesi;** hoja ilitolewa na mjumbe alitaka taarifa za kesi zitajwe baada ya taarifa hizo kutolewa kwa ufupisho ambapo taarifa hiyo ionyeshi kesi husika.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kuwa taarifa ya kesi zilizotolewa ni kesi ya Joseph Dotto Tambuko dhidi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Nachingwea kesi ya kupinga kubomoa vibanda vya biashara vilivyojengwa eneo la kituo cha mabasi Nachingwea. Kesi nyingine ni ya Saidi Abdallah Kalembo dhidi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Nachingwea kesi ya kupinga kubomoa nyumba iliyojengwa kwenye eneo la wazi, kesi ya Mkurugenzi Mtendaji dhidi ya NANRA CONSTRUCTIO CO, LTD ambayo ni kesi ya madai Halmashauri ikiomba kulipwa fedha ambazo mdaiwa alilipwa kwa kazi za ujenzi wa miundo mbinu ya Maji katika Kijiji cha Chiola na Notisi ya kushitakiwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Nachingwea na Ndugu Almasi Chikawe madai ya kazi ya nyongeza kandarasi ya ujenzi wa nyumba ya Mganga Zahanati ya Marambo.

**Zoezi la Ununuzi wa Vifaa;** hoja ilitolewa na mjumbe kuhusu zoezi la ununuzi wa vifaa mradi wa TASAF kunusuru Kaya Masikini, na njia zilizotumika kuwapata wazabuni kwa ujanja ujanja. Mjumbe aliongeza kwa kusema vifaa vimenunuliwa kwa bei za juu kuliko uhalisia.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kwa wajumbe kwa kusema kuwa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ilipata taarifa hizo ambapo ilifikia uamuzi wa kuunda timu ya kufuatilia utaratibu mzima uliotumika katika zoezi la ununuzi wa vifaa kwa sababu taarifa ilileta utata kiasi kamati ya fedha imeandaa timu itakayofuatilia zoezi zima la ununuzi wa vifaa na kuwaomba wajumbe hoja hiyo waiache wasiijadili kupisha timu teule ifanye kazi na kuwasilisha taarifa yake kwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

**Kituo cha kutoa Huduma inayohusu Matrekta;** Mjumbe baada ya kupitia taarifa kuhusu kituo cha kutolea huduma inayohusu Matrekta, mjumbe alitaka kujua kama Halmashauri inavyo vigezo vya kupata kituo na kuhoji kama kuna Wilaya zingine ziliingia kwenye ushindani.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kuwa wataalam kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Kitengo cha zana na kilimo baada ya kufanya ukaguzi kwenye Karakana yetu ya Matrekta iliyopo Idara ya Ujenzi, wariridhishwa na Karakana hiyo na kusema Wilaya inavyo vigezo kwa kuwa na eneo kubwa la kuweka Matrekta.

**2. KAMATI YA UJENZI, UCHUMI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa Kamati alitoa ripoti na kuwasilisha Muhtasri wa kikao cha tarehe 10.01.2017 ambao umethibitishwa.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavo

**Migogoro ya ardhi;** Mjumbe alisema kuhusu kushughulikiwa kwa migogoro ya ardhi kuwa migogoro ya Ardhi iliyosuluhishwa ingeainishwa kwenye taarifa. Mjumbe aliendelea kusema kamati inayokwenda kusuluhisha migogoro ifuate kanuni na sheria na maamuzi yazingatiwe.

**3. KAMATI YA ELIMU , AFYA NA MAJI**

Mwenyekti wa Kamati alitoa ripoti na kuwasilisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 10.01.2017 ambao umethibitishwa.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavyo

**Eneo la kujenga shule;** Hoja ilitolewa na mjumbe kutoa ombi la kupata eneo la kujenga shule ya Msingi Kata ya Boma, Mjumbe alisema Halmashauri ya Wilaya ifikirie na kushughulikia kupata eneo kwa ajili ya kujenga shule.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kuwa kulingana na jiografia ya Kata ya Boma hakuna eneo la wazi la kutosha kujenga shule linalomilikiwa na Halmashauri, labda eneo linalomilikiwa na Jeshi na kuongeza kuwa hoja ya kupata eneo upande wa jeshi ipo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Maelezo zaidi kuhusu kupata eneo kwa ajili ya Ujenzi wa Shule upande wa jeshi yalitolewa kuwa, kupata eneo jeshini haiwezekani labda liangaliwe eneo lingine.

**Usambazaji wa Maji;** hoja ilitolewa na mjumbe kuhusu tatizo la usambazaji/ uwekaji wa mabomba ya maji kwa wananchi mitaa ya Kalfonia, na maeneo ya Stendi mpya, ambapo mjumbe alisema utokaji wa maji sio wa kuridhisha na kuomba Idara iangalie katika maeneo hayo.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kwa kusema tatizo la huduma ya kufungiwa mabomba linatokana na kukosekana na vifaa (Mabomba) Mamlaka ya Maji MANAWASA, aidha wajumbe walisema Meneja wa Maji MANAWASA ni vyema awe anaalikwa kuhudhuria vikao vya Halmashauri kwa ajili ya kutolea ufafanuzi hoja za Maji zinazotolewa.

4. **KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Mwenyekiti wa Kamati alitoa ripoti na kuwasilisha Muhtasari wa tarehe 09.01.2017 ambao umethibitishwa.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa kama ifutavyo

**Kupatiwa msaada watoto wanaoishi kwenye Mazingira magumu;** hoja ilitolewa na mjumbe kutaka kujua watoto waliotambulika kuwa wanatoka kwenye mazingira magumu kama wamepatiwa vifaa na vifaa vya kielimu.

**Ufafanuzi;** ulitolewa kuwa watoto wote 42 wamepatiwa vifaa vya kielimu ambapo fedha ya nyongeza ilitoka mfuko wa jimbo ambazo ziliwezesha watoto hao wote kupatiwa msaada.

**HWN/MBK/MUHTASARI NA 93/2016 KUFUNGA MKUTANO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge Mkutano. Mwenyekiti alianza kwa kuwashukuru wajumbe kwa namna walivyoshiriki na kuchangia hoja katika Mkutano huo. Mwenyekiti aliendelea kwa kutaka maazimio yafanyiwe kazi. Mwenyekiti alilizungumzia ujenzi wa barabara ya Lami kutoka Nachingwea hadi Ruangwa ambapo alisema barabara hiyo itaunganishwa toka ilipoishia barabara ya Lami kuelekea Liwale jirani na Ofisi za Mamlaka ya Maji MANAWASA hadi eneo la Nangowe ambapo barabara itapanda na kutokea barabara ya Matangini- Ruangwa. Mwenyekiti alifunga mkutano saa 09.45 mchana.

**IMETHIBITISHWA**

................................ ................................
**MWENYEKITI** **KATIBU**

CHAIRMAN
NACHINGWEA DISTRICT COUNCIL

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NACHINGWEA

27-07-2017
..........................................
**TAREHE**